LAICOS VERNIANOS

LAICI VERNIANI
MANI APERTE PER AIUTARE

WALEI VERNIANI

VERNIAN LAITY

Walei Wanaverniana

Hati na safari ya kimalezi

YALIYOMO

- Idhini ya Chama uk. 3
- Katiba ya Chama cha “Walei Wanaverniana” uk. 4
- Waumini Walei uk. 9

Malezi ya Waumini Walei uk. 9

Malezi ya Walei Wanaverniana uk. 12

- Ahadi ya Uaminifu uk. 17
- Kitambulisho cha kiverniani uk. 18
- Hati ya Mkutano Mkuu wa IV uk. 19
- Hati ya Mkutano Mkuu wa V uk. 22
- Sala kwa Bikira Maria uk. 26

IDARA

YA MASHIRIKA YA KITAWA NA YA KITUME

Prot. n. I. 5-1/2004

IDHINI

Chama kilichoitwa “Walei Wanaverniana” cha Shirika la kitawa la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya asili la Ivrea, ambalo Makao Makuu yako katika Jimbo Kuu la Roma, ni Chama cha Waumini wenye nia ya kuishi karama ambayo Mama Antonia Maria Verna amewarithisha Masista wake, wakiwa wanaimwilisha katika maisha yao.

Wakiitikia mwaliko wa Kanisa, lakini pia wakiishi ndani ya ulimwengu, Wanachama wa “Walei Wanaverniana” wanashiriki lengo, karama na utume wa Shirika la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya asili la Ivrea.

Idara hii ya Mashirika ya Kitawa na ya Kitume, baada ya kupekua kwa makini Katiba iliyoandaliwa, hutamka kuwa Chama hiki ni tawi la Shirika na kupaswa kutambuliwa hivi na wote.

Kwa hati hii, pia, tunakabidhi kwa Mkuu wa Shirika pamoja na Kamati yake kazi ya kuidhinisha Katiba na pia kukubali mabadiliko yake ambayo yatahitajika kwenye mustakabali, wakiwa wanatoa taarifa kwa Kiti Kitukufu.

Hakuna kipingamizi kwa yaliyoandikwa.

Kutoka Vatikani, 18 Mei 2004,
Silvano Nesti, C.P.
Katibu Mkuu

sr. Enrica Rosanna, F.M.A. Katibu Mkuu Msaidizi

KATIBA YA CHAMA CHA WALEI WA KIVERNIANI
SEHEMU YA KWANZA
LENGO NA MUUNGO WA CHAMA

Ibara 1

Ndani ya familia ya Kiverniani, ambayo inapata picha yake kutokana na jina la Mama Antonia Maria Verna, pamoja na wale wote kwa njia moja au nyingine wanaopata mvuto wa pekee (Masista wa Shirika la Upendo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, Wamisionari wa Upendo, vikundi, vyama vya walei pamoja na muumini mmoja mmoja) wanajumuishwa pamoja katika jina la WALEI WA KIVERNIANI. Hiki ni chama binafsi cha waamini wa kikristo wanaopenda kumwilisha wito wao wa kikristo kwa kushiriki kikamilifu katika karama ya Shirika la Masista wa Upendo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya asili la Ivrea, mintarafu hali yao ya kilei, wakidumisha umoja kwa namna ya pekee na Masista wa Shirika hilo.

Wanachama kwa namna ya pekee wanapenda kujitahidi kuliishi Fumbo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha ya kikristo pamoja na kutoa mchango wake katika dhana nzima ya shughuli za kitume zinazofanywa na masista kwa upendo na katika asma nzima ya uinjilishaji.

Ibara 2

Tasaufi ya maisha ya Bikira Maria inamsukuma kila mwanachama kukuza ndani mwake ibada kwa Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, kwa kusherehekea kikamilifu Sherehe yake ya Kukingiwa dhambi ya asili, kusali kila siku pale inapowezekana Rozari takatifu, kujitahidi kuishi kikamilifu maisha ya kikristo, kila mtu kadri ya hali yake ya maisha na uaminifu katika majukumu yake ya kitawa, kwa kushiriki ibada ya Misa takatifu pamoja na maisha ya kisakramenti.

Tasaufi hii inapata mvuto wake wa pekee kutokana na lbara 2 na 3 ya Mwongozo wa Maisha ya Shirika la Masista wa Upendo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili la Ivrea.

Ibara 2: «Katika fumbo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, sisi tunaona na kutambua fumbo la mtu kujitoa bila kujibakiza kwa Mungu anayependa na kuokoa». Akiwa amejaa neema lakini pia yuko huru na zawadi ya kupendeza, Bikira Maria amejitoa kwa Mungu kwa namna ya pekee kabisa kwa sababu yeye ni Mama wa Neno wa Mungu aliyefanyika mwili akaunganika kikamilifu na Kristo Mkombozi na hatimaye kushiriki katika Fumbo la Ukombozi wa binadamu.

Ibara 3: «Ndani ya Bikira Maria tunapata picha kamili ya hali yetu ya maisha ya kuwekwa wakfu na utakatifu mambo ambayo tunaalikwa kuyaishi pamoja na nguvu kwa ajili ya shughuli za kitume. Kwa kutafakari fumbo lake tunachota ile karama ya kweli ya Shirika, tunajitahidi kujifunza kuwa jumuiya ambayo inajitoa kwa ajili ya Mungu na jirani. Kama Bikira Maria tunamwilisha ule upendo wa Kristo unaokomboa, kwa kujiachilia wazi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya jirani zetu».

Ibara 3

Wajibu wa kitume utatekelezwa katika kuwa na mtazamo wa pekee "*hasa kwa maskini na wahitaji*" tunaokutana nao na, kutoa muda na msaada, kulingana na nafasi ya kila mmoja, kwa utume wa upendo. Wajibu wa kitume wa uinjilishaji na katekesi unabidi uanze na Kristo, kama Baba Mtakatifu Yohane Paulo II amesisitiza katika Waraka wake *Tuingie Milenia mpya*, na unadai kulenga *"kipimo cha juu katika kuishi kila siku Ukristo wetu",* (*Tuingie Milenia mpya* 31); tena, unadai umakini katika malezi endelevu ya kiroho na utayari wa kujitoa kwenye kazi ya uinjilishaji na katekesi.

Kwa njia hii Walei wanawajibika kuishi wito wa utakatifu, tuliopewa katika Ubatizo, na pia wanawasaidia Wakristo wengine.

II - UONGOZI WA CHAMA

Ibara 4

Makao Makuu ya Chama cha Walei Wanaverniana yako Roma, *via della Renella 85*, kwenye Nyumba Kuu ya Shirika la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili la Ivrea. Uongozi wa Chama umegawanyika katika sehemu kuu tatu: **Mahalia, Kikanda na Kimataifa**.

4.1 Katika ngazi **Mahalia** kuna vikundi vinavyotambulika; kila kikundi kuongozwa na Mwenyekiti aliyechaguliwa na wanakikundi, kila baada ya miaka 4.

4.2 Katika ngazi **ya Kikanda** kuna Rais anayechaguliwa kila baada ya miaka minne na Mkutano Mkuu wa Kanda, unaundwa na Wanachama wote wa vikundi ambao wameweka ahadi. Rais wa Kanda anachaguliwa na zaidi ya nusu za kura zote.
Rais wa Kanda anasaidiwa na Washauri wawili, ambao wanachaguliwa vile vile na Mkutano Mkuu wa Kanda.
Uchaguzi utafanyika baada ya kuandaa vikundi na utasimamiwa na mmojawapo wa Kamati Kuu ya Chama au mwakilishi wa Rais Mkuu.
Mipaka ya Kanda inaamuliwa na Rais wa Chama akiwa na idhini ya Kamati yake.

4.3 Katika ngazi ya **Kimataifa**, kuna Rais anayesaidiwa na Washauri wanne, wanaochaguliwa kila baada ya miaka minne na Mkutano Mkuu.
Mshauri wa kwanza ni Makamu wa Rais na anaweza kumwakilisha Rais katika majukumu fulani ambayo Rais mwenyewe atampa na pia atachukua nafasi ya Rais wakati Rais hayupo au anazuiliwa kuwepo.

4.4 Baraza Kuu linalosimamia ushirika ni Mkutano Mkuu unaohakilisha Chama chote na unaoundwa na wakilishi wa lazima (Rais na Washauri Wakuu na Rais wa Kanda zote za kiverniani), pamoja na wakilishi wanaochaguliwa.
Mkutano Mkuu unafanyiwa kila baada ya miaka minne na una majukumu makuu yafuatayo:

- Kumchagua Rais Mkuu wa Chama pamoja na Washauri Wakuu wanne
- Kufanya tathmini ya maisha ya Chama
- Kuandaa mikakati kwa kipindi cha miaka minne.

Ibara 5

Kikundi chochote kitatambuliwa kikatiba pale tu kitakapopata ridhaa ya Rais wa Chama baada ya kushauriana na Washauri wake Wakuu. Ili kuweza kutambuliwa kikatiba, vigezo vifuatavyo havina budi kutiliwa maanani:

- ldadi ya wanachama isipungue watu kumi.
- Wanachama wasitawanyike mno katika maeneo ya kijiografia
- Wanachama wakusanyike kwa pamoja kadiri inavyowezekana ili kuweza kutekeleza majukumu ya Katiba.
- Kikundi kiwe na jumuiya ya Shirika la Masista wa Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili la Ivrea kama sehemu ya rejea.

Ibara 6

Kiongozi mahalia atakuwa ni kiungo cha ndani (yaani miongoni mwa vikundi mbalimbali, Rais wa Kanda na Rais Mkuu) pia na watu wa nje. Huyu ndiye mhusika mkuu katika kuilinda Katiba ya Chama. Ni mhamasishaji mkuu wa maisha ndani ya kikundi, katika mambo ya kiroho, ya kitume na katika kuleta maendeleo ya Chama chenyewe.

Ibara 7

Wajibu wa Rais wa Kanda ni sawa sawa na ule wa kiongozi mahalia, lakini katika ngazi yake ya uongozi. Ili kutekeleza wajibu huu Rais anasaidiwa na Washauri wake. Kwa namna ya pekee ni kazi yake, akiwa na idhini ya Kamati yake, kukubali maombi kimaandishi ya wanachama wapya, pamoja na kushughulikia masuala yaliyomo katika uwezo wake.

Ibara 8

Nyajibu za Rais na Kamati yake

8.1 Rais Mkuu ana majukumu, kwa mujibu ya Katiba hii, juu ya maisha na maendeleo ya Chama kizima na anahitisha Mkutano Mkuu. Kwa lengo hili anasimamia Katiba ifuatiwe. Katika kutekeleza majukumu yake anasaidiwa na Kamati yake.

8.2 Kwa namna ya pekee Rais Mkuu anapaswa kuwa na mawasiliano na Mama Mkuu wa Shirika la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili la Ivrea, hasa kwa yale yanayohusu uaminifu kwa Karama, roho, utume na malezi.

8.3 Ni jukumu la Rais Mkuu na Kamati yake kuchambua mapokezi ya Wanachama Wapya, ikihitajika kumwondoa mwanachama na kuwajibika na masuala muhimu ya Chama chenyewe.

III - KUPOKELEWA, KUTOLEWA, KUACHA CHAMA

Ibara 9

Ili kupokelewa kwenye Chama mwombaji sharti awe mtu (mwanaume au mwanamke, aliyeoa/kuolewa au mtu bila ndoa) na umri zaidi ya miaka 18, Mkatoliki safi na, baada ya malezi yafaayo, atawajibika ili kutekeleza kwa makini lengo la Chama pamoja na kufuata Katiba kwa kuweka ahadi ya uaminifu kwa maandishi ambayo yataandaliwa kwa nia hiyo; ikiwezekana ahadi hizi zifanyike ndani ya liturujia, hali ikiruhusu kwenye nyumba ya masista na zitakuwa zikirudiwa kila mwaka, ifikapo tarehe 8 Disemba.

Ibara 10

Mtu aliyepokelewa kuwa mwanachama anaweza kuondolewa kutoka kwenye Chama na idhini ya Rais Mkuu, akiwa hatekelezi majukumu yake bila kutoa sababu wala kurudia ahadi yake, baada ya kuonywa na Rais wa Kanda mara mbili kimaandishi au mbele ya mashahidi wawili.

Ibara 11

Mtu akiwa na sababu za kuacha Chama, ataongea na Mwenyekiti wake au na Rais wa Kanda yake.

IV- MAISHA YA CHAMA

Ibara 12

Chama kitasimamia kwa namna ya pekee malezi ya kikristo ya Wanachama, ili wajiandae vema zaidi kwa ajili ya kutekeleza malengo ya Chama chenyewe. Kwa ajili hiyo itaandaliwa mikutano ama semina za malezi, kwa kufuata mpango wa mwaka, chini ya usimamizi wa Rais Mkuu na Kamati yake.

Ibara 13

Mpango wa mwaka lazima uwe na tafakari ya kina (kiteolojia na kisaufi) juu ya wito na utume wa Walei; maandalizi ya kitume kwa ajili ya nyanja zilizopangwa kusaidia utume; somo juu ya roho ya familia ya kiverniani.

Ibara 14

Wanachama wanaitwa kufanya utume hasa pale ambapo wapo Masista wa Ivrea na wakishirikiana nao, huko hospitalini, mashuleni, maparokiani, katika umisionari na katika shughuli mbalimbali za sehemu husika, wakidumisha umoja na viongozi wa Kanisa mahalia na pia umoja na vyama vingine.

Ibara 15

Kila mwanachama awajibike kukuza maisha yake ya kiroho, kwa njia ya uaminifu kwa majukumu yake kama Mkristo na Mlei; kuwa na ibada ya pekee kwa Bikira Maria Imakulata, mintarafu hasa sala ya Rozari

Takatifu, ikiwezekana kila siku; kujiendeleza katika imani katoliki, hasa kwa kutafakari Maandiko Matakatifu, Katekisimu ya Kanisa Katoliki na usikivu kwa mafundisho ya Baba Mtakatifu.

Ibara 16

Kwa namna ya pekee yatasomwa na kutafakariwa Mafundisho ya Kanisa juu ya matendo ya "Upendo": kuhudumia, kuinjilisha, kufundisha, kuwatunza kwa namna ya pekee wahitaji (Rejea Miongozo 1823).

Ibara 17

Angalau kila baada ya miezi mitatu utengwe muda kwa ajili ya sala, mafungo, semina na tathmini.

Ibara 18

Anayependa, ataweza kushiriki sala, tafakari la Neno na matukio ya jumuiya ya masista.

V - UCHUMI

Ibara 19

Chama hiki hakina lengo la kujitafutia faida. Fedha zinazohitajika kwa ajili ya kufikia malengo ya Chama zinatoka kwenye michango ya Wanachama wenyewe au kutoka sehemu nyingine. Fedha hizo zinasimamiwa, katika ngazi mbalimbali, na Mweka Hazina, chini ya uangalizi wa viongozi husika.

VI. MSHIKAMANO NA SHIRIKA LA MASISTA WA UPENDO WA BIKIRA MARIA MKINGIWA DHAMBI YA ASILI LA IVREA

Ibara 20

Chama kinatekeleza lengo lake katika umoja na Masista wa Shirika la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili la Ivrea ambalo ni chanzo cha karama hii. Umoja huu unakidai Chama kushiriki kikamilifu katika maisha na tasaufi ya Shirika hili kwa kufahamu historia ya Shirika, tasaufi yake pamoja na utume wake.

Ibara 21

Mama Mkuu wa Shirika ndiye msimamizi mkuu wa karama ya Chama, malezi ya kiroho ya wanachama pamoja na kulinda utambulisho wa Chama; kwa namna ya pekee atawajibika kuhamasisha uwepo wa tathmini ya shughuli za kitume na yale ya kuyapatia kipaumbele; kazi hii itafanyiwa na akina Mama Wakuu wa Kanda, kwa ngazi ya kijimbo.

Ibara 22

Mama Mkuu wa Shirika anaweza kushiriki daima katika mikutano ya Kamati Kuu na Mkutano Mkuu wa Chama. Rais wa Chama daima anapaswa kumjulisha Mama Mkuu wa Shirika juu ya mwenendo wa Chama na kila mwaka, kwa lengo hili, atamtumia taarifa kimaandishi.

Ibara 23

Chama hakina budi kuhakikisha na kuona kwamba uwepo wa Masista ni jambo muhimu katika shughuli na maendeleo yao. Ni vyema kuhakikisha kwamba kila mtu aishi tasaufi yake mintarafu hali yake ya maisha. Ni vyema kutotoa mwanya wa ushirikiano katika mambo yale yasiyozingatia wito wa kifamilia na maisha ya walei na kwa upande mwingine wito wa maisha ya kitawa kwa masista.

VII - MALEZI YATOLEAYO NA PADRE

Ibara 24
Kwa upande wa malezi ya kiroho, ya kiimani na ya kitume, Chama kinaweza kupata msaada kutoka kwa padre.

VIII - HATIMA

Ibara 25
Katiba hii ni halali kwa Chama kizima, lakini inaweza kufanyiwa mabadiliko kidogo kuendana na mazingira ya majimbo husika. Mabadiliko hayo hayana budi kuidhinishwa na Rais wa Chama, baada ya kupata kibali kutoka kwa Washauri wake wakuu pamoja na Mama Mkuu wa Shirika la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili la Ivrea. Pale ambapo hakuna maelezo yaliyotolewa katika Katiba hii, zinafuatwa Kanuni za Sheria ya Kanisa.

Maamuzi ya Mkutano Mkuu wa tarehe 24.10.2015
Mkutano Mkuu ulijadili changamoto za sehemu zenye kikundi kimoja tu cha Walei wanaverniana. Mkutano Mkuu uliamua kuwa katika mazingira haya ya pekee, Rais Mkuu pamoja na Kamati yake wataunda huko Kikundi au Kanda; kwa sababu hiyo, itafuatwa itifaki ya Vikundi ama Kanda.

Roma, 3 Januari 2003; imebadilishwa na Mkutano Mkuu wa tarehe 29 Disemba 2007; imebadilishwa na Mkutano Mkuu wa tarehe 24 Oktoba 2015.

Kwenye Mkutano Mkuu wa tarehe 24-27 Oktoba 2019 vimepitishwa na kura zote vipengele vifuatavyo:

1) Kati ya Washauri Wakuu wanne, mmoja atahusika na malezi na mmoja na utume, baada ya kupata malezi yafaayo.
2) Kati ya Washauri wale wawili wa Kanda, ambao ikiwezekana inafaa watoke kwenye vikundi viwili tofauti, mmoja atahusika na malezi na mmoja na utume, baada ya kupata malezi yafaayo.
3) Kila kikundi kitakuwa na mwenyekiti ambaye atakuwa karibu na Kamati ya Kanda na ataweza kushiriki mikutano yao, akiwa amealikwa na Rais wa Kanda.
4) Wanachama wote watashiriki malezi na utume pamoja na matawi mengine mawili ya Familia ya kiverniani, kama yapo.
5) Kila Mlei Mverniani atauhaisha kikundi chake, kupitia ahadi yake ya kurudia kila mwaka, kushika vema wito wake kama Mlei na kwa kuhudhuria mikutano ya malezi na ya kitume.

WAUMINI WALEI

Waraka wa kichungaji ***Christifideles laici*** (CfL) wa Yohane Paulo wa II kuhusu *Wito na utume wa Walei katika Kanisa na katika ulimwengu*, Roma, 30.12. 1988.

Kutoka Injili ya Mathayo (Mt 20, 1-5a)

«Ufalme wa mbinguni unafanana na mtu mwenye shamba la mizabibu, ambaye alitoka asubuhi na mapema kuwaajiri wafanyakazi katika shamba lake. Akapatana nao kuwalipa fedha denari moja kwa siku, kisha akawapeleka katika shamba lake la mizabibu. Akatoka mnamo saa tatu asubuhi, akaona watu wengine wamesimama sokoni, hawana kazi. Akawaambia, 'Nendeni nanyi mkafanye kazi katika shamba la mizabibu, nami nitawapeni haki yenu. Basi, wakaenda.»

WAUMINI WALEI (…) ni sehemu ya Taifa la Mungu ambayo tunapata picha yake kwenye simulizi hili la wafanyakazi kwenye shamba la mizabibu, lililoelezwa kwenye Injili ya Mathayo.

Mfano huu wa kiinjili unapanua mbele yetu ukubwa wa shamba la Mungu na uwingi wa watu, wanaume kwa wanawake, ambao Yeye anawaita na kutuma ili wafanye kazi katika shamba hili. Shamba la mizabibu ni ulimwengu mzima (rejea Mt 13, 38), unaopaswa kubadilishwa kadiri ya mpango wa Mungu tukisubiri ujio wa mwisho wa Ufalme wa Mungu.

Mwaliko wa Bwana Yesu «*Enendeni hata ninyi katika shamba langu»* unaendelea kuita tangu siku ile: ni mwaliko kwa kila mwanadamu anayezaliwa katika dunia hii.

Nendeni hata ninyi. Mwaliko huu si tu kwa Wachungaji, mapadre, watawa, bali ni kwa wote: hata waumini walei wameitwa mmoja mmoja na Bwana, anayewapa utume kwa ajili ya Kanisa na kwa ajili ya ulimwengu mzima. Mtakatifu Gregori Mkuu anatukumbusha hayo akitafakari mfano wa wafanyakazi katika shamba la mizabibu: «Ndugu wapendwa, mwangalieni namna yenu ya kuishi na mkajiulize kama ninyi tayari ni wafanyakazi katika shamba la Bwana. Kila mmoja anathathmini anachofanya na kujiuliza kama anafanya kazi katika shamba la mizabibu la Mungu » (Rejea CfL 1-2).

MALEZI YA WAUMINI WALEI

… ili muzae matunda zaidi

(kutoka sura ya V ya waraka Christifideles Laici)

UKOMAVU ENDELEVU

57. Picha ya kiinjili ya mzabibu na matawi inaonesha tabia ya wito na utume wa waumini walei: wito *wa kukua, kuendelea kukomaa na kuzaa matunda zaidi na zaidi.*

Matawi yako hai endapo yanabaki pamoja na mzabibu: «*Anayekaa ndani yangu nami ndani yake anazaa matunda mema, kwani bila mimi hamwezi chochote*» (Yoh 15:5).

Wito wa Mungu unamwajibisha mwanadamu kukua, kukomaa, kuzaa matunda. Mwanadamu hawezi kutojibu, hawezi kuchukua jukumu lake. Jukumu hili ni muhimu na linatajwa na Yesu akisema: «Asiyebaki ndani yangu anatupwa kama tawi lililokauka na linalokatwa na kutupwa motoni» (Yoh 15: 6).

Katika mazungumzo haya kati ya Mungu anayeita na mtu anayejibu ndiyo kuna uwezekano, tena ulazima wa malezi endelevu ya waumini walei.

KUTAMBUA NA KUISHI WITO NA UTUME

58. Lengo la malezi ya waumini walei ni kutambua zaidi na zaidi wito wao na pia kuwa tayari kuuishi katika kutekeleza utume.

Mungu ananiita mimi na ananituma mimi kama mfanyakazi katika shamba lake la mizabibu; ananiita mimi na ananituma mimi kufanya kazi kwa ajili ya ujio wa Ufalme wake katika historia ya wanadamu: wito huu na utume huu vinadhihirisha hadhi na wajibu wa malezi yote, ambayo yana lengo la kutambua kwa furaha na shukrani hadhi hiyo na pia vinalenga utekelezaji wa wajibu huu, kwa uaminifu na ukarimu.

Tangu umilele Mungu ametufikiria sisi na ametupenda kama watu wa pekee, tofauti na wengine, akiwa anamwita kila mmoja wetu kwa jina lake, kama Mchungaji mwema «anayemwita kila kondoo kwa jina lake» (Yoh 10, 3). Lakini mpango wa milele wa Mungu unadhihirika kwa kila mmoja wetu katika historia ya maisha ya kila mmoja na matukio yake, maana yake unadhihirika taratibu: siku baada ya siku.

Ili kuelewa mapenzi halisi ya Mungu juu ya maisha yetu, tunahitaji usikivu wenye utayari na utii wa Neno la Mungu na neno la Kanisa, sala ya kimwana na ya kudumu, kumtegemea uongozi wa kiroho, kuchambua kiimani vipawa na talanta tulizopewa na pia kuchambua mazingira ya kijamii na kihistoria tunapoishi.

Kwenye maisha ya kila mwamini mlei *ziko nyakati za pekee* ili kupambanua wito wa Mungu na kupokea utume wake: kati ya nyakati hizo uko wakati wa *ujana.* Ila tusisahau kuwa Bwana, kama yule mwenye shamba wa Injili, anatuita -ili kutekeleza Mapenzi yake- *saa zote* za maisha: ndiyo maana kukesha ni tabia msingi na ya kudumu ya kila mfuasi.

Si suala tu la *kujua* lile ambalo Mungu anataka kwetu katika kila tukio la maisha. Ni lazima *kutekeleza* lile ambalo Mungu analitaka, kama anavyotukumbusha Maria, Mama wa Yesu, katika neno lake kwa watumishi huko Kana: «Fanyieni lote atakalowaambieni» (*Yoh* 2, 5). Ili kutenda kadiri ya Mapenzi yake Mungu inabidi kuwa waaminifu kwa mapenzi hayo na kuwa na *uwezo*, tena na *uwezo zaidi*. Kwa kweli, kwa neema ya Bwana, ambaye haishindwi kamwe, kama Mtakatifu Leo Mkuu anavyosema: "Yeye aliyetoa cheo atatoa nguvu!"; lakini pia na ushirikiano na uwajibikaji wa kila mmoja wetu.

Hii ndio kazi ya kushangaza na ya kuhitaji ambayo inawangojea waamini walei wote, Wakristo wote, bila kukoma: kujua zaidi na zaidi utajiri wa imani na Ubatizo na kuyaishi haya yote kwa utimilifu unaozidi. Mtume Petro, akizungumzia kuzaliwa na ukuaji kama hatua mbili za maisha ya Kikristo, anatuhimiza: "Kama watoto wachanga, mtamani maziwa safi ya kiroho, ili kukua nayo kuelekea wokovu" (1 Pt 2: 2).

MALEZI JUMUISHI NA SHIRIKISHI

59. Katika kutambua na kuishi wito na utume wao, waumini walei wanapaswa kulelewa katika *umoja*, kama *wanakanisa* na pia kama *wanadamu.* Hakuna maisha mawili: ya «kiroho», na tunu na mahitaji yake; na upande mwingine ya «kiulimwengu», yaani maisha ya kifamilia, kikazi, kijamii, kisiasa na kitamaduni. Tawi linalounganika na mzabibu ambao ni Kristo mwenyewe, linazaa matunda yake katika kila sekta ya shughuli zake na maisha yake. Nyanja zote za maisha ya Walei ni sehemu ya mpango wa Mungu, ni mahali pa kihistoria penye ufunuo na penye utekelezaji wa Mapendo ya Yesu Kristo kwa sifa ya Baba na kwa utumishi wa ndugu wote. Kila shughuli, kila hali, kila wajibu -kwa mfano, utaalamu na ushirikiano katika kazi, upendo na majitoleo katika familia na katika kuwalea watoto, huduma ya kijamii na kisiasa, pendekezo la ukweli katika nyanja ya utamaduni - ni fursa za kufanya "mazoezi thabiti ya imani, matumaini na mapendo".

VIPENGELE VYA MALEZI

60. Vipengele vingi na vilivyoratibiwa vya *malezi jumuishi* ya waamini walei viko ndani ya muhtasari huu wa maisha.

Hakuna shaka kwamba malezi *ya kiroho* lazima ichukue nafasi ya upendeleo katika maisha ya kila mmoja, anayeitwa kukua bila kukoma katika uhusiano wa karibu na Yesu Kristo, kulingana na Mapenzi ya Baba, kwa kujitolea kwa ndugu katika upendo na haki.

Katika nyakati zetu ni muhimu sana malezi ya *kimafundisho* ya waamini walei, si tu kwa lengo la kuimarisha imani yao, lakini pia kwa hitaji la «kutetea tumaini» lililo ndani yao mbele ya ulimwengu na changamoto zake ngumu.

Kwa sababu hiyo ni lazima kuwa na *katekesi endelevu*, tofauti kadiri ya rika mbali mbali na kadiri ya hali tofauti za maisha. Pia, ni muhimu kuendeleza *utamaduni wa kikristo*, ili kujibu maswali ya msingi yanayowasumbua wanadamu na jamii ya nyakati zetu.

Kwa namna ya pekee, hasa kwa waumini walei wanaowajibika katika nyanja za kijamii na kisiasa, ni muhimu sana kufahamu zaidi *Mafundisho ya kijamii ya Kanisa.*

… Katika mazingira ya malezi jumuishi na shirikishi ya waamini walei, ukuaji wa kibinafsi katika *maadili ya kibinadamu* ni muhimu sana kwa hatua yao ya kimisionari na ya kitume. Kwa maana hii, Mtaguzo Mkuu uliandika: "(walei) wanapaswa pia kuzingatia uwezo wa kitaalamu, hali ya familia na uraia na sifa hizo zinazohusu uhusiano wa kijamii, ambayo ni uaminifu, roho ya haki, uwazi, nidhamu, nguvu ya roho, ambazo zikikosekana haiwezekani pia kuwa na maisha halisi ya Kikristo».

Katika kuelekea ukomavu wa maisha yao, ambayo kwa pamoja ni kielelezo cha umoja wa maisha yao na hali ya kutimiza vyema utume wao, waamini walei wataongozwa na kuungwa mkono na Roho Mtakatifu, Roho wa umoja na uzima.

WASAIDIZI WA MUNGU MLEZI

61. Je! Ni maeneo gani na njia gani za malezi ya waamini walei? Je! Ni *watu* na *jumuiya* gani wanaoitwa kuchukua jukumu la malezi jumuishi na shirikishi ya waamini walei?

Kama vile kazi ya malezi ya kibinadamu imeunganishwa sana na baba na mama, vivyo hivyo malezi ya Kikristo hupata mizizi na nguvu zake kwa Mungu Baba ambaye anawapenda na kuwalea wana wake. Ndio, *Mungu ndiye mwalimu wa kwanza na mkuu wa Taifa lake*, kama kinavyosema kile kifungu kizuri cha Wimbo wa Musa (Kumb 32, 10-12; taz. 8, 5).

Kazi ya malezi ya Mungu inafunuliwa na kutimizwa katika Yesu, Mwalimu, na hufikia moyo wa kila mtu kwa uwepo wa nguvu wa Roho. *Mama Kanisa* anashiriki katika kazi ya malezi ya Mungu, yenyewe na katika viungo vyake. Hivi ndivyo *waamini walei wanavyoundwa na Kanisa na katika Kanisa*, katika ushirika wa pamoja na ushirikiano wa washiriki wake wote: makuhani, watawa na waumini walei. Kwa hivyo jamii yote ya Kanisa, katika washiriki wake wote, hupokea matunda ya Roho na inashirikiana nayo kikamilifu.

Kwanza kabisa, anayelea ni *Kanisa lote,* ambalo ndani yake Baba Mtakatifu ndiye mlezi wa kwanza wa waumini walei. Kwake, kama mrithi wa Petro, ni utumishi wa «kudhibitisha ndugu katika imani», akiwafundisha waumini wote yale ya muhimu kuhusu wito na utume wa Kikristo. Waumini walei wanapaswa kusikiliza kwa utulivu na upendo si tu neno lake la moja kwa moja, lakini pia neno lake lililowasilishwa kupitia nyaraka za Idara mbali mbali za Kiti Kitakatifu.

Kanisa moja na katoliki lipo ulimwenguni kote katika *Makanisa mahalia*. Ndani ya kila Kanisa mahalia, Askofu ndiye mwenye jukumu la kibinafsi kwa waamini walei: anapaswa kuwaunda kupitia tangazo la Neno, maadhimisho ya Ekaristi na ya sakramenti, uhamasishaji na uongozi wa maisha yao ya Kikristo.

Ndani ya kila Kanisa mahalia ziko na zinafanya kazi *Parokia*, na kila parokia ina jukumu muhimu kwa malezi ya karibu na ya kibinafsi ya waamini walei. Kwa kweli, katika uhusiano ambao unaweza kufikia watu binafsi na vikundi kwa urahisi zaidi, parokia inaitwa kuwalea washiriki wake katika kusikiliza Neno, katika mazungumzo ya kiliturujia na kibinafsi na Mungu, katika maisha ya misaada ya kidugu, na kuwafanya waone na kuonja hali ya ushirika wa kikanisa na uwajibikaji wa kimisionari.

MAENEO MENGINE YA MALEZI

62. Hata *familia ya Kikristo*, kama "Kanisa la nyumbani", ni shule ya asili na ya msingi kwa malezi ya imani: baba na mama hupokea kutoka kwa sakramenti ya Ndoa neema na huduma ya malezi ya Kikristo kwa watoto wao, na kuwashuhudia na kuwarithisha pamoja maadili ya kibinadamu na ya kidini. Kwa kujifunza maneno ya kwanza, watoto pia hujifunza kumsifu Mungu, ambaye wanahisi kuwa karibu nao kama Baba mwenye upendo na mlezi; kwa kujifunza ishara za kwanza za upendo, watoto pia hujifunza kufungua moyo wao kwa wengine, wakigundua maana ya maisha ya mwanadamu katika zawadi ya kibinafsi. Maisha ya kila siku ya familia halisi ya Kikristo ni "maang'amuzi ya kwanza ya Kanisa", yanayopata uthibitisho na maendeleo katika kuwashirikisha

watoto kwenye uwajibikaji katika jamii pana ya Kanisa na ya jamii. Wanandoa wa Kikristo na wazazi wanapokua katika ufahamu kwamba "Kanisa lao la nyumbani" linashiriki katika maisha na utume wa Kanisa la ulimwengu, ndivyo watoto wengi wataweza kufundishwa "maana ya Kanisa" na watahisi uzuri wote wa kutoa nguvu zao kwa ajili ya kuutumikia Ufalme wa Mungu.
Sehemu muhimu za malezi pia *ni shule na Vyuo Vikuu vya Katoliki*, na pia vituo vya upyaji wa kiroho ambao leo unazidi kuenea.
Hata *vikundi, vyama na harakati* vina nafasi katika malezi ya waumini wakei: kila moja na mbinu zake, vina nafasi ya kutoa malezi endelevu yanayojikita katika maang'amuzi ya kitume na pia fursa ya kukamilisha, kujumuisha na kubainisha mafunzo ambayo wanachama wao wanapata kutoka kwa watu wengine na jamii.

MALEZI SHIRIKISHI

63. Malezi si faida ya wachache, bali haki na wajibu wa wote. Mababa wa Sinodi walisema: «Wote wapate nafasi ya malezi, hasa maskini ambao wao wenyewe wanaweza kuwa chemchemi ya malezi kwa watu wote», na pia waliongeza: «Kwa ajili ya malezi itumike mbinu ambayo imsaidie kila mtu kuishi wito wake wa kibinadamu na wa kikristo».
Katika kazi ya malezi kuwa fikra ambazo ni za muhimu sana na pia zinaleta matunda. Kwanza kabisa fikra ya kwamba hakuna malezi ya ukweli na yenye mafanikio bila mtu kuamua mwenyewe kuchukua wajibu wa malezi: malezi ni kujilea.
Tena, fikra ya kuwa kila mmoja wetu ni mwanzo na mwisho wa malezi: zaidi tunavyolelewa, zaidi tunavyohisi haja ya kuendelea na malezi, na pia zaidi tunavyolelewa, zaidi tunavyohisi umuhimu wa kuwalea wengine.
Ni muhimu sana kuwa na imani ya kwamba malezi, yakipata msaada kutoka kwenye njia na mbinu za kisayansi, yatasaidia zaidi endapo yatakuwa tayari kupokea *utendaji wa Mungu:* tawi ambalo haliogopi kukatwa na mwenye shamba litazaa zaidi, kwake na kwa manufaa ya wengine pia.

MALEZI YA WALEI WANAVERNIANA

Muwe waaminifu kwa wito wenu!

Antonia Maria Verna

"Wanachama kwa namna ya pekee wanapenda kujitahidi, kwa mfano wa Mama Antonia Maria, kuliishi Fumbo la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, wakimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya maisha ya kikristo pamoja na kutoa mchango wao katika dhana nzima ya shughuli za kitume zinazofanywa na masista kwa upendo na katika asma nzima ya uinjilishaji." (Katiba n°1)

Mpango mkuu wa Malezi umegawanyika katika sehemu kuu mbili:

A - Malezi ya kwanza kwa waombaji

B -Malezi endelevu kwa Wanaverniana wenye ahadi

A – MALEZI YA KWANZA

"Ili kupokelewa kwenye Chama mwombaji sharti awe (mwanaume au mwanamke, aliyeoa/kuolewa au mtu bila ndoa) na umri zaidi ya miaka 18, Mkatoliki safi na, baada ya malezi yafaayo, atawajibika ili kutekeleza kwa makini lengo la Chama pamoja na kufuata Katiba kwa kuweka ahadi ya uaminifu kwa maandishi ambayo yataandaliwa kwa nia hiyo; ikiwezekana ahadi hizi zifanyike ndani ya liturujia, hali ikiruhusu kwenye nyumba ya masista na zitakuwa zikirudiwa kila mwaka, ifikapo tarehe 8 Disemba. " (Katiba, 9)

Kipengele namba 9 cha Katiba kinaongea kuhusu "malezi yafaayo" kabla ya kuweka ahadi. Neno "yafaayo" yanamaanisha kuwa inabidi Chama kiwajibike kuwapa waombaji malezi bora ili kuwawezesha kuelewa vizuri maana na nyajibu za ahadi.

➢ *Kipindi cha malezi*

Urefu wa hiki kipindi kinaweza kuwa tofauti, lakini si chini ya miaka miwili (2). Kama kuna kesi za pekee lazima zichunguzwe na Rais wa Kanda na Kamati yake, kwa makubaliano na Rais Mkuu.

➢ *Wenye wajibu wa malezi*

Pamoja na yale yaliyoandikwa kwenye Katiba: *Rais Mkuu na Kamati yake ni mwenye wajibu wa malezi, na Mama Mkuu wa Shirika ni msimamizi wa malezi hayo,* lakini katika Kamati Kuu ya Chama kuna Mshauri anayeshughulika malezi, na hivyo hivyo kwenye Kamati ya Kanda.

Katika kila kikundi na kila Kanda ni vizuri kumchagua *Mlei Mverniani* mwenye busara, uadilifu, unyenekevu na unyofu, mwenye roho ya ibada, mwenye kuaminika, ambaye anaweza kusindikiza safari ya malezi ya wanaoanza safari ndani ya Chama. Mtu huyu anaweza kusaidiwa na sista katika kazi hiyo. Endapo, katika kikundi cha kiverniani, asipatikane mlei mverniani mwenye kushika wajibu huu, sista au padre anaweza kusaidia kazi hii.

Mwombaji apokelewe kwenye *kikundi,* kama ndugu katika Kristo, ili kuanza kufahamika, na ili kung'amua mtindo wa maisha ya familia ya kiverniani na kuanza safari ya kuwa mshuhuda mwaminifu.

➢ *Tathmini*

Katika malezi ya kwanza iwepo nafasi ya tathmini, hasa kwa upande wa nyajibu zinazotolewa kwa waombaji. Tathmini hii inapaswa kuwa nafasi ya kujadiliana kirafiki, ili mwombaji aweze kueleza changamoto na wasiwasi zake na kusaidiwa kuendelea na safari yake ya kiverniani.

Mwombaji anapaswa kusaidiwa:

1. Kusoma zaidi

- ✓ Mada ya maisha kama wito
- ✓ Mada ya wito wa kikristo

2. Kujua
   - ✓ Wajibu wake na nafasi yake kama Mlei ndani ya Kanisa
   - ✓ Kujua wito na utume wa Mlei Mverniani

3. Kujua
   - ✓ Maisha na utume wa Mama Antonia
   - ✓ Roho na karama ya Shirika la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili la Ivrea

4. Kujua Katiba

Mlei anayemsindikiza mwombaji kwenye safari yake ya malezi, akutane naye mara kwa mara, ili safari hiyo iwe na manufaa ya kiroho, ya kimasomo na pia ya kivitendo.
Ni vizuri kupanga wajibu halisi kwa mwombaji.
Ni vizuri kupanga nafasi za kukutana na kikundi kwa ajili ya malezi na mafungo.
Ni vizuri kutamadunisha malezi kadiri ya tamaduni mahalia na pia yaendane na hali ya mtu anayefanya safari hii.
Endapo kuna Mlei mwenye maandalizi ya kutosha na anayependa kuelewa kwa undani zaidi vipengele fulani fulani kuhusu karama, roho, Maandiko Matakatifu, imani, basi, Mwenyekiti ataomba msaada kwa watu wenye taaluma hizo, akiwa amemshirikisha pia Mshauri mwenye wajibu wa malezi.

N.B. Kuwa mwombaji/mtakaji hamlazimishi mtu kuweka ahadi, kwani ahadi ni uamuzi wenye ukomavu na uhuru.

1 – MAISHA NI WITO

A – WITO WA MAISHA

- ✓ Zaburi 139 (138) *Ewe Bwana unanijua na kunichunguza…*
- ✓ *Mungu amemwumba mtu kwa sura na mfani wake…* (Mwa 1:27).

Somo la kitabu cha Mwanzo, katika sura zile zinazoongelea uumbaji wa mwanadamu.
Somo la KKK nn.355-384.

B – WITO WA IMANI KUPITIA UBATIZO

«Maisha yote ya mwamini Mlei yanapaswa kumsaidia kujua yale mapya kabisa yatokanayo kwenye Ubatizo, Sakramenti ya imani, ili aweze kuwajibika katika imani kadiri ya wito aliopewa na Mungu» (*Christifideles Laici* n.10)

Sakramenti (KKK 1212 - 1658)
Amri kumi (KKK 2083 – 2550)
Sala za kikristo (KKK 2559 – 2856)

Vitabu vya rejea: Biblia na KKK

TUNAWAJIBIKA:
- kushiriki Misa kila Jumapili
- kushiriki mikutano (vikao, semina nk) ya kikundi
- kutenda matendo ya huruma kila siku, nyumbani, kazini nk

2 – UTUME WA MLEI NDANI YA KANISA

Kusoma kwa undani *utume wa Mlei ndani ya Kanisa*

- KKK, nn. 897 – 913.
- Kusoma Waraka wa kitume *Christifideles Laici.*

TUNAWAJIBIKA:
- Kushiriki shughuli za kiparokia: vyama, utume, matukio nk…

3 - MAISHA NA UTUME WA MWENYEHERI ANTONIA MARIA

Roho na karama ya Shirika la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili la Ivrea ni chemchemi ya utume wa Mlei Mverniani.

Kusoma
- Maisha, roho na karama ya Mwenyeheri Antonia Maria
- Kutafakari namna ya kutekeleza Miongozo 4 ya Mama Antonia na miongozo ya Mlei Mverniani;
- Kutafakari Fumbo la Kukingiwa dhambi ya asili kwa Bikira Maria

Vitabu vya rejea
- Kitabu cha Maisha ya Mama Antonia
- Kitabu cha Maandishi ya Mama Antonia
- *SCIC, Cachu ya majitoleo*

TUNAWAJIBIKA:
- Kung'amua upendo unaojitoa bila kujibakiza katika kutoa na kupewa: kutoa muda, usikivu, uvumilivu, msamaha, msaada bila kudai chochote na pia kwa furaha, hasa kwa wahitaji zaidi;
- Kushiriki matendo ya huruma: parokiani, kwa masista au sehemu nyingine, kwa manufaa ya maskini;
- Kusali kila siku tendo moja la Rozari Takatifu.

Kusoma kwa makini Katiba na Ahadi.

B – MALEZI ENDELEVU
Kwa walioweka tayari Ahadi

Wenye wajibu

Pamoja na yale yaliyoandikwa kwenye Katiba: *Rais Mkuu na Kamati yake ni mwenye wajibu wa malezi, na Mama Mkuu wa Shirika ni msimamizi wa malezi hayo,* lakini katika Kamati Kuu ya Chama kuna Mshauri anayeshughulika malezi, na hivyo hivyo kwenye Kamati ya Kanda.

Nyajibu

Ni muhimu sana kuwa Mlei aliyeweka ahadi ajitahidi kukua daima katika maisha ya kiroho, kupitia:
- Misa Takatifu, hata za kila siku ikiwezekana;
- Kusoma na kutafakari Maandiko Matakatifu;
- Kusali Rozari kila siku;
- Ibada ya kuabudu, Njia ya Msalaba...

Katika malezi endelevu ni muhimu:
- Kutafakari upya na kwa undani zaidi mada za malezi ya kwanza.

(Vitabu vya rejea daima ni Biblia na KKK);
- Kutafakari Hati za Kanisa, Mafundisho ya Baba Mtakatifu nk.;

- Kutafakari zaidi juu ya Mwanzilishi, Maandishi yake, Karama (Vitabu vya rejea ni vile vilivyotajwa kwenye kipengele cha 3 cha malezi ya kwanza, na vinaweza pia kuongezwa vingine ama Hati au vitabu kuhusu Fumbo la Kukingiwa dhambi ya asili kwa Bikira Maria;
- Kufuata *Mpango wa kiroho* wa mwaka, unaotoka kwenye Shirika na ambao unawashiriki pia Wamisionari wa Upendo.

Wanachama hawana budi kuishi kiadilifu Ahadi na kujitambua kama sehemu hai ya Familia ya kiverniani.

Ni lazima kila Mlei ashike kwa ndani Karama ya Mama Antonia, na kuiweka kwenye matendo halisi, mintarafu utume wa upendo na matendo madogo madogo ya upendo usiojibakiza, akiwa kwenye Familia, kwenye kikundi chake, parokiani nk…
Katika kila mahali Mverniani anaitwa kumtangaza Kristo na Injili yake yenye matumaini, ufukara, udugu na furaha, hata Msalabani, na kuwa chombo cha amani, umoja, huruma.
Mlei Mverniani aige ujasiri, ubunifu na utakatifu wa Mwanzilishi!

Ahadi ya uaminifu ya Walei Wanaverniana

Kwa sifa na utukufu wa Mungu
katika Roho Mtakatifu
mimi ……
naupyaisha ahadi ya
Ubatizo wangu na kujitoa
kufuata kiaminifu
Katiba cha Chama cha Walei Wanaverniana.
Nikifuata mfano wa M.heri Mama Antonia,
nataka kuishi roho
ya Shirika,
kulingana na wito wangu kama Mlei
na katika umoja na Masista
na Wamisionari wa Upendo
nikitoa pia mchango wangu
katika utume wao wa
uinjilishaji na
utumishi, hasa wa maskini.
Neema ya Roho Mtakatifu
na maombezi ya Maria Imakulata
na wa M.heri Mama Antonia
vinisaidie kuwa mwaminifu
kwa ahadi yangu.
Amina.

Kitambulisho cha kiverniani

Miongozo ya Mama Antonia ya mwaka 1823

1. Kuwauguza mchana na usiku na
kuwasaidia kadiri ya nguvu zao
wagonjwa wa jinsia zote mbili,
wakiwa na ugonjwa wowote
hata wa kuambukizwa au ukoma,
na hiyo bila kujibakiza na bila kudai malipo,
hasa kwa maskini.

2. Kuwafundisha katekesi wasichana hasa maskini,
konventini na parokiani,
hasa wakati wa Kwaresima,
na hiyo bila kujibakiza na bila kudai malipo.

3. Kuwafundisha kusoma na kuandika
wasichana wote bila ubaguzi hasa wale maskini,
na hiyo bila kujibakiza na bila kudai malipo.

4. Kuwatunza kwa namna ya pekee wasichana wote yatima na walioachwa,
hasa wale wasiokuwa na mali yoyote,
ili kuwasaidia kupata maisha yanayowafaa,
kadiri ya wito wao na vipaji vyao, na kuwapa tena chochote
kwa riziki yao, kulingana na mazingira na uwezo wa jumuiya.

Miongozo ya Walei Wanaverniana

5. *Kuishi umoja na Wanaverniana wote na pia Familia ya kiverniani yote, tukikomaa pamoja katika imani, kwenye mwanga wa Injili.*

6. *Kuishi upendo usiojibakiza na usiodai malipo, tukivuviwa na Fumbo la Kukingiwa dhambi ya asili ya Bikira Maria.*

7. *Kuishi maisha yetu na wito wetu, katika ukweli, uimara na udumifu, tukijitoa kabisa kwa wengine wahitaji.*

8. *Kuthamini malezi ya kiroho; kuyaishi kila siku kwa vitendo vya upendo, unyenyekevu na unyofu. YOTE "A GRATIS"*

A. KITAMBULISHO CHA KIVERNIANI

Walei wanaverniana wanajitambua kama jumuiya ya waumini wanaowajibika kujiendeleza kiimani, kuishi Injili na tunu za majitoleo, utayari, mshikamano, heshima, upendo, unyenyekevu, unyofu, hasa kwa maskini, jinsi alivyoishi Mama Antonia, wakivuviwa na Fumbo la Kukingiwa dhambi ya asili kwa Bikira Maria.

Katika Mkutano Mkuu tumesisitiza sana hayo yote na pia tulitambua kuwa sisi tuna wito, na wito huu unatudai jibu la kweli, lenye imani, lenye udumifu utokanao kwenye tafakari la kila siku la Neno la Mungu, kumwabudu Yesu aliye hai katika Ekaristi na aliyejitoa Msalabani. Mlei Mverniani ni mtu "*anayemtafuta Yesu*" kwa furaha na akiwa na hamu ya kukutana naye.

Ndiyo maana kila mmoja wetu anaitwa kuupyaisha na kuuhaisha mahusiano yake na Mungu katika sala (Neno la Mungu, Ekaristi), katika jumuiya yake ya kiverniani kwa kutafuta nafasi za kuishi udugu wetu na kuhusiana na kila ndugu, hasa maskini, jinsi alivyotuagiza Mama Antonia *massime ai poveri*.

Katika kushirikishana "mwongozo elekezi wa Mkutano Mkuu" yamedhihirika wazi yale mazuri ambayo tunayatekeleza, pamoja na yale yanayokwamisha safari.

Yale hasi yanatupa changamoto, wakati yale chanya yanatusukuma kuota juu ya mustakabali ujao, wenye uwezekano wa kujitoa zaidi, wa kushuhudia kwa ujasiri na kutangaza Injili, wa kuwashirikisha vijana katika malezi ya kikristo na ya kiverniani, wa kuwa na mshikamano zaidi kati ya vikundi.

Tafakari juu ya wito wetu, kuamini kuwa kila mmoja anapaswa kuutikia kwa kuwajibika, majitoleo katika utume vinatusukuma kutumia nguvu zetu zote na malezi yote tuliyopewa kwa ajili ya kujitoa kwa vijana na uhamasishaji wa miito.

Tunahitaji ujasiri, tunahitaji kujihisi sehemu hai ya Familia moja, tunahitaji kuwa na utayari, bidii, roho ya sadaka katika majitoleo, hadi kuwa "*mbegu inayokubali kufa ili wengine waishi*" , ili kumpeleka Yesu kwa wote wanaomtafuta.

B. MUSTAKABALI WETU

Kutafakari karama

Sisi tunamtafuta Yesu; Injili ni mwongozo wetu wa maisha. Namna yetu ya kuishi Injili ni namna ile ya karama ya Mama Antonia. Kila Mlei Mverniani hana budi ya kutafakari karama na kuweka misingi mizuri mintarafu kusoma, kushirikisha, kusali na kutenda:

- Kupitia maelezo yanayojitosheleza na tafakari ya kiteolojia, kiroho, kimafundisho na kimaisha;
- Kwa kushirikisha ndani ya kikundi na wakati wa sala utajiri wa karama na maang'amuzi ya kimisionari;
- Kwa kushiriki shughuli za kimisionari ambazo zinadhihirisha karama yenyewe na pia kwa kuwa karibu na watu (Masista, Wamisionari wa Upendo na Walei) wanaoshuhudia karama, ingawa na madhaifu yao;
- Kwa kujitahidi katika kila kikundi kuwa na sista mmoja mlezi, mwenye uwezo wa kushirikisha roho ya kiverniani;
- Kwa kuendelea kujibidiisha katika "miradi ya upendo" ambayo yanaonesha umisionari wa karama, tukifanya kazi pamoja na "Verna fraternitas Onlus" na vikundi vingine pia.

Kujihisi sehemu ya Familia moja

Mlei Mverniani lazima ajihisi kuwa yeye ni *sehemu hai ya* Familia iliyoanzishwa na Mama Antonia, hata akiwa anashiriki pia vikundi vingine vya majitoleo vya mazingira yake. Upekee wake utakuwa karama tuliyorithishwa na Mwanzilishi.

Hata matumizi yenye busara ya vyombo vya mawasiliano (redio, runinga, magazeti nk) katika ulimwengu ambao "kuonekana" ni muhimu, yanaweza kuwa njia ya kutangaza *namna yetu ya upendo usiojibakiza ya kuishi Injili.*

Malezi

Wote tunaamini kuwa malezi ni ya msingi na pia yanatofautiana kadiri ya tamaduni zetu mbali mbali. Malezi yanapaswa kuwa *endelevu na yenye malengo*, yaani tofauti kwa ajili ya wenye ahadi tayari na wale wanaoanza.

Malezi yanahusu

- Kukomaa katika imani tuliyopewa kwenye Ubatizo, tukimtafuta Yesu daima katika Neno, Ekaristi na katika ndugu pia,
- Kukomaa katika wito na utume kwa kufuata Injili na karama ya kiverniani,
- Kujua kusoma nyakati zetu na changamoto zao katika mwanga wa imani.

Malezi yanafanyika kwenye Vikundi, kwenye Kanda na pia katika ngazi ya Kimataifa.

Katika vikundi malezi yanapatikana kwa njia ya mahudhurio ya kudumu, ushirikiano wa kidugu, kujitambua kama sehemu ya kikundi, uwazi ndani ya kikundi na mshikamano na mawasiliano na vikundi vingine.

Katika ngazi ya Kanda malezi yanapatikana kwa njia ya mikutano, semina, nyakati za sala na mpango wa pamoja. Ni muhimu kusali pamoja na kutenda pamoja, *tukishikamana.*

Katika ngazi ya kimataifa, Kamati Kuu, licha ya kuandaa *mpango wa kiroho wa kila mwaka*, ingepaswa kupanga siku mbili za malezi, huko Roma na kuwaalika Wanaverniana, jinsi ilivyofanyika kwenye miaka ya mwanzo.

Pia Kamati Kuu inapaswa:
a) Kuandaa kijarida juu ya Katiba, pamoja na nyongeza za Mikutano Mikuu;
b) Kuandaa jarida inayoeleza ahadi;
c) Siku ya sala ya Familia nzima ya kiverniani (matawi yote matatu), ili kuombea Familia wote kwa pamoja, kwa maombezi ya Mama Antonia;
d) Kutoa maelezo juu ya vikundi, Kanda, shughuli zao na malezi yao, kupitia tovuti yetu ya www.laiciverniani.net .

Hayo yote yatafanyika kwa nguvu itokanayo kwenye *Neno la Mungu*, tukipata malisho kwenye *Ekaristi*, tukiwa na upendo kwa *ndugu* na *jumuiya* yenye tabia za Mama Antonia: unyenyekevu, unyofu na upendo usiojibakiza.

Vijana

Pale ambapo kuna vikundi vya vijana hatuna budi:
- Kupanga shughuli zifaazo ili kuamsha vipaji vyao kiutu na kiroho;
- Kuwavuta vijana kwa Yesu na Injili, tukiwa tunaishi karama yetu;
- Kuwatazama kwa namna ya pekee wanandoa vijana, wanaowafikia masista wetu kwenye shule zao, kwa kuwashirikisha kwenye shughuli zetu, kuwafanya wajiulize maswali, na pia kwa kupanga mikutano ili

kuwaelezea juu ya roho ya kiverniani na juu ya shughuli za Chama chetu. Mfano mzuri wa Wanaverniana walio imara na mapokezi mazuri ni ufunguo unaofungua moyo wa vijana.

Kujitambua kama Familia

Ili tuboreshe mawasiliano na mahusiano kati ya vikundi na kanda, kwa lengo la kuelewa changamoto zao na kujitambua zaidi kama Familia ya kiverniani, Kamati itakutana katika sehemu mbali mbali, angalau huko Italia. Kila kikao cha Kamati kitadumu siku tatu, ili kuwezesha Wanakamati kutembelea kanda tofauti, kushiriki shughuli nao na pia kuwaalika Rais na Wanakamati wa Kanda husika.

Mtindo wa maisha

"Kumtafuta Yesu" kutakuwa lengo kuu la Wanaverniana wote kwa miaka minne ijayo, tukifanya maamuzi kulingana na karama ya kiverniani.

Tutamtafuta Yesu, *kwa furaha na kwa kuwajibika,*
Tutamtafuta Yesu, *tukiwa na imani kwa Maongozi ya Mungu*, tukijua kuwa yeye hawezi kumwacha mtu,
Tutamtafuta Yesu, *kwa furaha* ya ukweli

- katika kutafakari Neno la Mungu, binafsi na katika jumuiya/kundi;
- katika Ekaristi, Misa na Sakramenti;
- Katika udugu, tukiwa wabunifu katika kupanga nafasi ya kujitoa kwa wengine. Ndugu tunapaswa kukutana nao tukiwa na roho ya kimisionari na tukiwa na macho yanayotambua mahitaji ya kila mmoja, kama anavyotuomba Baba Mtakatifu.

Pia, tutakutana na ndugu huko Msalabani, endapo tunapokea hata sisi misalaba yetu, kwa uvumilivu wa kikristo na roho ya kiinjili.

KWA NJIA HII CHAMA KITAKUWA HAI, KITAZAA MATUNDA NA KITAKABIDHIANA IPASAVYO NA CHANGAMOTO ZA NYAKATI ZETU.

KARAMA: Zawadi ya Roho Mtakatifu kwa ajili yetu

- *Karama ni zawadi ya Roho Mtakatifu ambayo Mungu amelijalia Shirika la Masista wa Upendo wa Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili la Ivrea na pia amemshirikisha kila Mverniani;*
- *Msingi wa karama ya Mwenyeheri Antonia Maria Verna ni unyofu, upendo na "gratuità", yaani hali ya kujitoa bila kujibakiza na bila kudai malipo au shukrani;*
- *"Gratuità" yetu si wazo au nadharia fulani; inajikita katika Upendo wa Mungu na jibu letu kwake, kwa kufuata kielelezo cha Bikira Maria;*
- *Kadiri ya mafundisho ya Mama Antonia, Upendo ni kuishi pamoja na Kristo, kwa ajili ya Kristo na katika Kristo. Upendo wetu unaanza na sala na malezi, unafungua mioyo yetu, unatusukuma kuwasaidia maskini wote, wa kimwili na wa kiroho;*
- *Inatubidi kujua karama yetu kupitia malezi, kuiishi katika ushuhuda, kushirikishana, ili tuishi katika umoja na amani, tukishinda vikwazo.*

KWA HIYO TUNAWAJIBIKA:

1**. KUFAHAMU ZAIDI** karama yetu kwa kupitia malezi endelevu na imara, tukisaidiwa na wale wanaoishi karama hiyo;

2. **KUMWILISHA** karama yetu kwa ubunifu katika nyakati zetu na mazingira yetu;

3. **KUISHI** karama yetu katika matendo ya huruma: kuwalisha wenye njaa, kuwatembelea wagonjwa, kufundisha katekesi, kuwasaidia wahitaji na wanaoteseka;

4. **KUSHIRIKISHANA** karama kwa kupitia mbinu zinazofaa, kwendana na nyakati;

5. **KUSHUHUDIA** karama tukifuata kila siku kwa furaha na uaminifu Miongozo minne (4) ya Mama Antonia na Miongozo minne (4) ya kiverniani.

CHAMA:
Upinde wa mvua wa Antonia Maria Verna, wenye rangi mbali mbali

- *Chemchemi ya wito wa Walei Wanaverniani iko katika Ahadi ya Ubatizo na Karama ya Mama Antonia;*
- *Kama Walei Wanaverniana tunaitwa kuwa imara katika imani, wito, upendo;*
- *Chama cha Walei Wanaverniani kinafanya kazi kwa kuzingatia malezi endelevu, kikifuata Mwongozo wa Mama Mkuu wa Shirika na Kamati yake na kwa kutekeleza Miongozo ya Mama Antonia na ya kiverniani na pia kikijitahidi kupambana na changamoto ngumu za kijamii;*

- *Namna ya kuishi ya Familia ya kiverniani inadhihirika katika fadhila zifuatazo: unyenyekevu, uchangamfu, furaha, udugu, uwazi, unyofu na ukarimu katika kushirikishana vipaji vyetu.*

KWA HIYO TUNAWAJIBIKA:

1. **KUKUTANA** kwenye kundi na pamoja na vikundi au matawi, kwa roho ya kifamilia;

2**. KUWA MWANGA** katika giza, kama Mama Antonia, tukiishi kila siku wosia wake;

3. **KULEA** viongozi katika Roho, viongozi wenye moyo wa kutumikia;

4. **KUHAMASISHA** Chama cha Walei Wanaverniana na utume wake mintarafu vipeperushi na mengineyo yaliyoandikwa kwa lugha mbali mbali;

5. **KURITHISHA** tunu za Mwanzilishi kwa vijana na kuwahamasisha wajiunge na Chama, kupitia matukio yanayowavuta na pia kupitia "fomula ya ahadi" inayowafaa;

6. **KUSAIDIA** Wanachama wajisikie nyumbani kwa kupitia malezi, matukio na hata sherehe za pamoja;

7. **KUCHAGUA** kila mwaka "Miradi ya Upendo", pamoja na Masista na Wamisionari wa Upendo, kwa kuwajibika kutoa hela kwa ajili hiyo na kuihamasisha kwa ubunifu.

KULETA MATUMAINI KATIKA ULIMWENGU WA LEO AMBAO NI CHANGAMOTO KWETU

- *Matumaini ni zawadi ya Roho Mtakatifu, yanafungua macho yetu na mioyo yetu na kuangaza giza ya historia yetu na ulimwengu wetu wa leo.*
- *Katika ulimwengu usiofahamu Injili wala mafundisho ya Kanisa Katoliki, Mama Antonia anatukumbusha kuwa utume wa kwanza wa upendo ni kumpeleka Kristo kwa wanadamu na wanadamu kwa Kristo.*
- *Katika hali ya umimi na upweke ya ulimwengu wa leo, Mverniani anajitahidi kuishi Injili ya udugu na kufuata mfano wa Mama Antonia, aliyewapenda watu wote: "Watawatambua kwa sababu ya upendo wenu kwa watu wote".*
- *Kila Mverniani anajitahidi kuwa mtu mwenye matumaini, mtu aliyepanda na kutunza mbegu ya matumaini katika maisha yake na anajitahidi kuipandikiza kwenye matendo yake yote.*
- *Upendo usiojibakiza wa Mama Antonia unamsukuma Mverniani kuwasaidia maskini, watoto na wazee wenye shida: "Watawatambua kwa matunda yenu".*

KWA HIYO TUNAWAJIBIKA:

1. **KUJIKABIDHI** kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, anayevunja kuta zote na anayevuma anakotaka.

2**. KUSALI** zaidi, kama watu binafsi, kifamilia na kama kundi, ili tupambanue vizuri namna tunavyopaswa kuishi karama ya Mama Antonia.

3. **KUJILEA** kiimani, kufundisha katekesi kwa bidii, kuboresha uinjilishaji wetu na kufanya huruma iwe kiini cha uinjilishaji huo.

4. **KUFUNDISHA** katekesi, kuanza kabisa na maisha na baadaye na maneno, katika parokia, jumuiya, familia, tukiweka kipaumbele kwa vikundi vya vijana, kundi linalotupa changamoto lakini ambalo linahitaji kuwa na mifano ya watu wazima waaminifu na imara katika imani.

5. **KUBUNI** matukio kwa ajili ya kuishi udugu wetu kama kundi, familia, parokia: matukio hayo yanasaidia kufahamiana zaidi na kusaidiana zaidi, hasa nyakati ngumu.

6. **KUOMBEANA** katika Kundi na Chama na kuwa karibu kiroho: kusali pamoja na kufanya kazi pamoja ili tujenge roho ya kifamilia na kukutana kwa njia hiyo na Yesu Mwalimu.

7. **KUSHIRIKISHANA** na Parokia, Vikundi na Vyama vingine ili kupeleka Neno na Matumaini kwa wagonjwa, wazee na watu wapweke wanaohitaji matumaini.

8. **KUISHI** matumaini. Matumaini yawe:

▪ Msukumo wa aliye mpweke na mwenye huzuni

▪ Msukumo wa anayejitoa kwa watu, bila kujali mazingira magumu

▪ Msukumo wa anayetaka kurithisha imani kwa watu wengine na kwa sababu hiyo yuko tayari kupambana na changamoto

9. **KUCHANGIA** mipango ya Upendo (yaani ya kuwasaidia maskini n.k.) ya Chama na ya parokia pia.

FAMILIA MOJA KATIKA ISHARA YA MATUMAINI

▪ *Sisi ni Familia moja, kwa sababu tunashiriki karama moja, karama ambayo Roho Mtakatifu amemjalia Mwenyeheri Antonia Maria Verna; kila tawi linaishi karama hiyo hiyo kadiri ya wito wake, kama Mtawa, kama Mlei Wakfu au Mlei. Maisha ya kiroho ya kiverniani yanatuonjesha furaha ya kuishi upendo usiojibakiza, unyofu na unyenyekevu katika namna yetu ya pekee, tukichota nguvu kwenye Ekaristia, Msalaba na Bikira Maria Mkingiwa dhambi ya asili.*

▪ *Kwa kufuata ibara namba 5 ya Katiba yetu, kila kundi la Wanaverniana liko karibu – pale ambapo panawezekana- na jumuiya ya Masista wa Upendo wa Bikira Maria mkingiwa dhambi ya asili; kundi linajitahidi kushirikiana pia na Wamisionari wa Upendo na watu wengine wenye mapenzi mema. Tunaheshimu tofauti za miito yetu na kufanya Familia yetu ya kiverniani iwe na umoja, ubunifu, mshikamano, ushirikiano na upendo kwa Mama Antonia.*

▪ *Ni muhimu kushirikishana talanta zetu za kimalezi na kiutendaji, kiroho na kiakili. Ni muhimu pia kushikamana hata kwa kutumia vizuri vyombo vya mawasiliano na pia kwa kuwa na hija za pamoja katika sehemu asilia za kiverniani (alipoishi Mwanzilishi).*

<u>KWA HIYO TUNAWAJIBIKA:</u>

1. **KUSOMA** zaidi karama na maisha ya kiroho, kwa kutumia mbinu zote tulizo nazo katika vikundi vyetu na ikiwezekana pia pamoja na Masista na Madada wa Upendo, ili kukuza na kudhihirisha zaidi roho yetu ya kifamilia (Familia yenye umoja, ubunifu, ushirikiano, uhusiano, upendo);

2. **KUWAJIBIKA** zaidi na kudumisha mawasiliano na mahusiano mazuri na wote na hasa katika mazingira yenye changamoto na umaskini;

3. **KUTAFUTA** fursa za kuwa pamoja kama Familia ya kiverniani, katika sala ama sherehe; tuwe na ukarimu pia na watu wa karibu, hata kama si Wanaverniana;

4. **KUFANYA** utume pamoja, pale ambapo panawezekana, tukitekeleza pamoja Miongozo minne (4) ya Mama Antonia “hasa kwa maskini”;

5. **KUFIKIRI** katika uwingi na si umimi;

6. **KUACHANA** na tofauti zetu na kuwajibika kuishi mshikamano, kwa manufaa ya watu wanaotaka ushuhuda wetu wa umoja.

Sala kwa Bikira Maria

Ewe Bikira mtakatifu sana,
Mama wa Kristo na Mama wa Kanisa, kwa heshima na taadima,
tunajiunga na Magnificat yako,
wimbo wako wa upendo na shukrani.

Pamoja nawe tunamshukuru Mungu,
ambaye «huruma yake ni kwa wote, kizazi hata kizazi»,
kwa ajili ya wito wa ajabu na utume pana wa waumini walei,
walioitwa kwa jina na Mungu ili waishi naye, katika umoja wa upendo na wa utakatifu,
na wawe wote kitu kimoja ndani ya familia kubwa ya Wana wa Mungu,
waliotumwa ulimwenguni kote kutangaza mwanga wa Kristo na kueneza moto wa Roho Mtakatifu, mintarafu maisha yao ya kiinjili.

Ewe Bikira wa Magnificat,
uijaze mioyo yao na shukrani na ari kwa ajili ya wito huu na utume huu.
Kwa unyenyekevu na moyo mkuu
wewe umejitambua kama
«mtumishi wa Mungu»:
utujalie utayari wako
wa kumtumikia Mungu
na kwa wokovu wa ulimwengu.
Upanue mioyo yetu ili
tupokee Ufalme wa Mungu na tutangaze Injili kwa kila kiumbe.

Katika moyo wako wa kimama
unabeba hatari nyingi na mateso mengi ya wanadamu wa nyakati zetu.
Lakini pia unabeba matarajio yao mema, tunu zao, manendelo yao katika njia ya wokovu.
Ewe Bikira mjasiri,
utujalie uhodari na utujalie pia imani kwa Mungu,
ili tuwe na uwezo wa kushinda vipingamizi vyote vya utume wetu.
Utufundishe kupambana na maulimwengu tukiwajibika kikristo na tukiwa na matumaini kwa ujio wa Ufalme wa Mungu, wa ujio wa mbingu na dunia mpya.

Wewe uliyebaki kusali pamoja na Mitume ukisubiri ujio wa Roho wa Pentekoste,
uombe tena ujio wake juu ya Waumini wote Walei,
wanaume kwa wanawake, ili wajibu kweli kweli wito wao, kama matawi ya mzabibu wa kweli, wakiwa wameitwa kuzaa matunda mema kwa uhai wa ulimwengu.

Ewe Bikira na Mama,
utuongoze na utusaidie ili daima tuhisi kama wana halisi wa Kanisa la Mwanao na tuweze kuchangia katika kujenga hapa duniani jamii ya ukweli na upendo, kadiri ya mpango wa Mungu na kwa ajili ya utukufu wako.
Amina. (*Kutoka Christifideles laici*)